SHULE YA SEKONDARI YA ST. ANTHONY – MBAGALA
(SHERIA ZA SHULE KWA WANAFUNZI)

UTANGULIZI: Ifahamike kwamba:-

- Shule ya Sekondari ya St. Anthony, ni shule ya **KUTWA**; lakini ina **HOSTELI** kwa ajili ya wanafunzi wa kike tu. Hosteli hiyo, iko ndani ya eneo la shule. Kwa hiyo basi:-

  (a) Hakuna jengo au nyumba iliyopo nje ya shule inayotambuliwa na shule kama makazi halali ya wanafunzi wa shule hii.

  (b) Wanafunzi wote watapaswa kuja shuleni wakitokea nyumbani kwa Wazazi / walezi wao.

  (c) Si ruhusa kwa mwanafunzi kukaa katika hosteli au nyumba ya kupanga isiyotambuliwa na shule.

  (d) Wanafunzi wa kike (**WASICHANA**), wanaweza kupata nafasi katika HOSTELI ya shule.

- Sheria hizi za shule zinalenga katika kumpatia mwanafunzi malezi bora; yaani kumwandaa vema kitaaluma na kinidhamu, ili kumwezesha kuwa raia mwema, aliye tayari kutumia uwezo wake wote kutumikia jamii inayomzunguka na Taifa kwa ujumla.

1. **TAALUMA:** Dira ya shule hii ni kuwa '**Kituo cha Taaluma na Nidhamu Bora**' na hatimaye kuwa shule bora na ya kuigwa Tanzania. Dhima ya shule ni '**Kutoa Elimu Bora Iliyokamilika (Holistic Quality Education**);' na kwa njia ya elimu hiyo, kuwakomboa vijana **kiroho, kimwili na kiakili**. Ili kufanikisha haya, ni lazima:-

(a) Kila mwanafunzi ahudhurie masomo kwa muda wa **siku mia moja tisini na nne (194)** kwa mwaka, ukiondoa Jumamosi, Jumapili na sikukuu za kitaifa.

(b) Kama kutakuwa na sababu za msingi za mwanafunzi kutofika shuleni, ni jukumu la mzazi/mlezi kufika mwenyewe kutoa taarifa kwa mkuu wa shule au walau kutoa taarifa ya maandishi kwa uongozi wa shule, mapema iwezekanavyo.

(c) Endapo mwanafunzi atakuwa hajahudhuria shuleni kwa muda wa siku tatu mfululizo, uongozi wa shule utamwita mzazi/mlezi wake kuja kutoa maelezo kwa nini mwanae hakufika shuleni. Asipokuwa na maelezo ya kuridhisha, mwanafunzi atachukuliwa hatua kali za kinidhamu, ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo kwa kipindi cha siku ishirini na moja (21) au zaidi.

(d) Endapo mwanafunzi atakuwa hajafika shuleni kwa siku 21 mfululizo, bila taarifa kwa Mkuu wa shule, mwanafunzi huyo atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe.

(e) Kila mwanafunzi awe ameingia darasani na kukaa katika kiti chake kabla ya mwalimu wa somo kuingia na kuanza kufundisha.

(f) Mwalimu aingiapo darasani wanafunzi wote wasimame na kumsalimia.

(g) Wanafunzi wote wawe kimya wakimsikiliza mwalimu wakati akifundisha isipokuwa mwalimu akiuliza swali, akiruhusu mjadala au maigizo darasani.

(h) Kila mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote kwa mujibu wa ratiba ya siku.

(i) Kila mwanafunzi afanye mazoezi na mitihani yote anayopewa na walimu wa masomo mbalimbali katika muda aliopewa.

(j) Kila mwanafunzi afikie wastani wa asilimia arobaini na tano (45%), kila mwisho wa mwaka wa masomo. Mwanafunzi atakayeshindwa kufikia kiwango hicho, atalazimika kukariri darasa. Kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita, wastani huo (45%) ni kwa masomo matatu ya msingi (Principal subjects).

(k) Mwanafunzi yeyote ambaye atakwepa kufanya mitihani au zoezi la somo lolote la kidato husika bila ruhusa iliyoidhinishwa na Mkuu wa shule, atapewa alama ya (0) katika somo hilo na alama hiyo itajumlishwa katika kutafuta wastani wake wa mwisho wa muhula au mwaka.

(l) Mwanafunzi haruhusiwi kuiba mitaihani kutoka kwa mwanafunzi mwenzake au kwenda chumba cha mtihani na majibu yaliyoandikwa kwenye karatasi, nguo rula n.k. au kuongea na mwanafunzi mwenzake kwenye chumba cha mitihani wakati mtihani ukifanyika. Atakayebainika kukiuka sheria hii ya shule, atapaata adhabu ya kusimamishwa masomo na hatimaye kufukuzwa shule.

(m) Kila mwanafunzi awe na daftari la mazoezi/majaribio kwa kila somo.

2. **NIDHAMU:** Shule ya Sekondari ya St. Anthony inaamini kuwa Nidhamu Bora ni Ufunguo wa Taaluma Bora. Kwa hiyo, inahimiza sana juu ya umuhimu wa wanafunzi kuwa na nidhamu bora. Kama sehemu ya nidhamu bora, ni lazima:-

(a) Kila mwanafunzi awe amefika shuleni kabla ya saa moja na nusu asubuhi akiwa katika sare rasmi ya shule iliyo safi.

(b) Kila mwanafunzi awahi kuhudhuria Mkutano wa Asubuhi na mchana (School Assembly) au mikutano ya asubuhi ya darasa kwa siku na wakati husika.

(c) Kila mwanafunzi awepo mahali husika kwa mujibu wa ratiba ya siku hiyo.

3. **AFYA NA USAFI:** Afya na Usafi ni sehemu muhimu ya Taaluma na Nidhamu bora. Kama watu wanenavyo: Akili njema hupatikana katika mwili wenye afya (***Mens sana in corpore sano)*** Kwa hiyo, ni lazima:-

(a) Kila mwanafunzi aonekane nadhifu wakati wote.

(b) Mwanafunzi ashiriki katika kusafisha na kutunza mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na kufagia /kudeki vyumba vya madarasa, kuondoa buibui, kufuta vumbi kwenye vioo, milango, madirisha n.k. kila atakapotakiwa kufanya hivyo.

(c) Kila mwanafunzi atunze vifaa vya, vya kufanyia usafi, atakavyokabidhiwa. Upotevu au uharibifu wa vyombo hivyo utagharimiwa na mwanafunzi ambaye atakuwa amehusika na uharibifu au upotevu wa vifaa hivyo.

(d) Wasichana hawaruhusiwi kujiremba, kama kupaka kucha rangi, kupaka midomo rangi, kupaka wanja, kunyoa kipara, kunyoa nyusi, kuvaa pete, hereni, bangili, mikufu, kuweka dawa kwenye nywele, kuwa na nywele ndefu, kucha ndefu n.k.

(e) Wavulana hawaruhusiwi kuwa na ndevu, masharubu, sharafa, kuvaa bangili, kuweka dawa kwenye nywele, kuvaa mikufu, kuvaa mlegezo, kunyoa kipara.

4. **SARE YA SHULE**:

(a) **Wanafunzi wa kiume (kidato cha 1 – 4): watavaa:** -

(i) Suruali ya kijivu au kaptula ya khaki na shati jeupe la mikono mifupi. Ni lazima shati liwe na nembo ya shule kwenye mfuko. Nembo hiyo isiwe ya kubandikwa.

(ii) Viatu veusi vya ngozi vyenye visigino vifupi, visivyo na mapambo ya aina yeyote na viwe vinafungwa na gidamu (kamba) nyeusi. Mabuti hayaruhusiwi.

(iii) Ni lazima viatu vivaliwe na soksi ndefu nyeupe, ziwe safi na zisiwe na mapambo.

(iv) Suruali au kaptula ifungwe kwa mkanda mweusi.

(b) Wanafunzi wa kike (Kidato cha 1 – 4): Watavaa:-

(i) Sketi ya kijani kibichi. Ni lazima urefu wake uwe chini ya magoti.

(ii) Shati jeupe la mikono mifupi. Ni lazima liwe na nembo ya shule kwenye mfuko wa shati. Nembo hiyo isiwe ya kubandikwa.

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi.ni lazima viatu viwe na visigino vifupi, na visiwe na mapambo ya aina yeyote na viwe vinafungwa kwa gidamu (kamba) nyeusi. Mabuti hayaruhusiwi.

(iv) Ni lazima viatu vivaliwe na soksi ndefu nyeupe, safi zisizo na mapambo.

(c) **Wanafunzi wa kiume (kidato cha V – VI): Watavaa:-**
(i) Suruali ya bluu iliyokolea (dark blue)

(ii) Shati jeupe la mikono mifupi, lenye nembo ya shule kwenye mfuko na isiwe ya kubandika.

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi. Ni lazima viatu viwe vya kufungwa kwa gidamu (kamba); vyenye soli fupi na visiwe na mapambo ya aina yeyote. Mabuti hayaruhusiwi.

(iv) Soksi ndefu, safi, zisizo na mapambo.

(v) Mkanda wa suruali uwe mweusi.

(d) **Wanafunzi wa kike (Kidato cha V – VI): Watavaa:-**
(i) Sketi ya bluu iliyokolea (dark blue)

(ii) Shati jeupe la mikono mifupi, lenye nembo ya shule kwenye mfuko na isiwe ya kubandika.

(iii) Viatu vya ngozi vyeusi. Ni lazima viatu viwe na soli fupi, viwe vya kufungwa na gidamu (kamba);na visiwe na mapambo yeyote. Mabuti hayaruhusiwi.

(iv) Soksi nyeupe ndefu, safi, zisizo na mapambo.

N.B sare zote (isipokuwa viatu, soksi na mkanda) zinapatikana shuleni.

5. **DINI:** Shule inaheshimu uhuru wa kuabudu kama ulivyoainishwa katika ibara ya 19 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kwa hiyo:-

(a) Kila mwanafunzi ataruhusiwa kuamini na kushiriki katika shughuli za dini yake au madhehebu yake ili mradi shughuli hizo zisiathiri sheria na taratibu nyingine za shule; hususani taratibu za kitaaluma na kinidhamu.

(b) Bila kuathiri uhuru wa kuabudu uliotajwa katika kipengele cha 5 (a), shule haitaruhusu mwanafunzi yeyote kubadili dini yake bila ridhaa ya maandishi toka kwa wazazi/walezi wake.

6. **MATIBABU:** Shule ina Zahanati ambayo hutoa huduma ndogo ndogo za matibabu kwa kuchangia gharama. Kwa hiyo:-

(a) Mwanafunzi atakayetakiwa kupata matibabu nje ya shule wakati wa masomo ni lazima awe amepitia Zahanati ya shule kwanza, na kupewa ruhusa ya maandishi ya Tabibu. Aidha, atapaswa kumtaarifu mwalimu wake wa darasa na mwalimu wa zamu, kisha apitie ofisi ya Nidhamu kupata kibali cha kwenda nje ya shule.

(b) Mwanafunzi anatakiwa kuwa mwazi na mkweli kuhusu hali yake kiafya, wakati wa kujiunga na shule na wakati wote atakapokuwa katika shule hii. Kasoro zote za kiafya alizo nazo ziandikwe kwenye fomu ya maombi ya kujiunga na shule ili kumwezesha kupata huduma muhimu pindi atakapohitaji.

(c) Likizo zote za ugonjwa zitatolewa na mkuu wa shule tu.

7. **TABIA NA MWENENDO**

(a) Mwanafunzi anatakiwa kuwasalimu wafanyakazi wote wa shule atakaokutana nao ndani na nje ya shule.

(b) Mwanafunzi anatakiwa kupokea /kutii amri zote halali zitolewazo na utawala wa shule bila ubishi.

(c) Mwanafunzi **HARUHUSIWI** kutumia lugha ya matusi.

(d) Ni marufuku kupiga kelele au kuleta usumbufu wa aina yoyote darasani au nje ya darasa.

(e) Ni marufuku mwanafunzi kutoka nje ya shule wakati wa masomo bila ya ruhusa toka kwa Mkuu wa shule au waandamizi wake.

(f) Kila mwanafunzi atawajibika kutunza mali yake binafsi pamoja na ile ya shule na kutoa taarifa kwa utawala wa shule endapo mali hizo zitaharibiwa/kuibiwa.

(g) Mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na vitu vya thamani kubwa vinavyoweza kuathiri tabia na mwenendo wake kitaaluma na kinidhamu; kama vile simu za mkononi, redio, kamera, sistimu ya video, kompyuta ndogo (laptops) au fedha nyingi kuliko mahitaji yake ya siku; bila ya ruhusa ya mkuu wa shule.

(h) Ni marufuku mwanafunzi kuiba mali ya mwenzake au ya shule au mali ya jamii inayozunguka shule na ya jamii yote kwa ujumla wake.

(i) Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza.

(j) Ni marufuku kuhamisha kiti/dawati /taa,swichi kutoka darasa moja kwenda mahali pengine bila kibali cha mwalimu wa darasa.

8. **MAKAZI YA MWANAFUNZI:** Kama ilivyokwishaelezwa katika UTANGULIZI, Shule ya Sekondari ya St. Anthony, ni shule ya **KUTWA**; lakini ina **HOSTELI** kwa ajili ya wanafunzi wa kike tu. Hosteli hiyo, iko ndani ya eneo la shule. Kwa hiyo basi:-

(1) Hakuna jengo au nyumba iliyopo nje ya shule inayotambuliwa na shule kama makazi halali ya wanafunzi wa shule hii.

(2) Wanafunzi wote watapaswa kuja shuleni wakitokea nyumbani kwa Wazazi / walezi wao.

(3) Si ruhusa kwa mwanafunzi kukaa katika hosteli au nyumba ya kupanga isiyotambuliwa na shule.

(4) Wanafunzi wa kike (**WASICHANA**), wanaweza kupata nafasi katika HOSTELI ya shule.

9. **MIPAKA YA SHULE:** Mipaka ya shule ni **"UKUTA"** unaozunguka shule.

(i) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.

(ii) Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali/ruhusa maalumu:- (a) Chumba cha walimu (Staff Room); (b) Maabara; (c) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

10. **SEHEMU AMBAZO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUONEKANA.** Ni marufuku kabisa kwa mwanafunzi kuonekana sehemu zifuatazo:-

(a) Vilabu vya pombe (Bars, Night clubs)

(b) Majumba ya starehe (Cinema Halls; Disco Halls n,k)

(c) Nyumba za kufikia wageni (Guest house)

11. ADHABU: Mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule akitenda moja au zaidi ya makosa yafuatayo:-

(a) Wizi wa aina yoyote.

(b) Uasherati na vitendo vyote vya kujamiana au kuleta hisia za kujamiana.

(c) Uvutaji bangi, uvutaji sigara, ulevi wa pombe ya aina yoyote pamoja na utumiaji wa madawa ya kulevya.

(d) Kuiba mitihani, kutazamia mitihani kutoka kwa wanafunzi wenzake au kwenda katika chumba cha mtihani akiwa na majibu yalioandikwa kwenye karatasi, nguo, rula n.k. au kuongea na mwenzake akiwa ndani ya chumba cha mtihani wakati mtihani ukifanyika.

(e) Kupigana na wanafunzi/wafanyakazi shuleni.

(f) Kutumia lugha ya matusi kwa wanafunzi au wafanyakazi.

(g) Kuruka ukuta wa shule.

(h) Kuhujumu au kuharibu kwa makusudi mali ya shule.

(i) Kuandika maandishi kwenye kuta za shule, kuta za madarasani, kuta za vyooni au kwingineko.

(j) Kuoa au kuolewa.

(k) Kutoa mimba au kushiriki katika kutoa mamba.

(l) Kupata mimba au kumpa mimba mwanafunzi.

(m) Kukataa adhabu iliyotolewa na utawala wa shule.

(n) Kushindwa kubadili mwenendo/tabia baada ya kuonywa na utawala wa shule, kwa maandishi.

12. HITIMISHO:

(1) Pamoja na sheria hizi, wanafunzi wa kike (wasichana) watakaokaa katika HOSTELI YA SHULE; watapaswa kusoma, kuelewa na kutekeleza sheria za nyongeza za Hosteli ya Shule.

(2) Utawala wa shule unaweza kubadili sheria hizi wakati wowote kwa lengo la kuboresha mwenendo na tabia ya wanafunzi kitaaluma na kinidhamu.

SHERIA HIZI ZINAPATIKANA PIA KATIKA TOVUTI YA SHULE: **www.stanthonys.ac.tz**